



SHIYANGA REGION CO-PERATIVE UNION (1984) LTD
P. O. BOX 349, SHINYANGA, TEL/FAX 255 28 2762525
Email:info@shireculimited.co.tz Website:www.shireculimited.co.tz

KUMB. NA.SRCU/TB/39/VOL.II/116

TAREHE : 22/04/2026

A. TANGAZO LA KOTESHENI

1. Chama kikuu cha Ushirika Mkoa wa Shinyanga ni Chama kilichosajiliwa kwa **Na.AFF-SHY-SHY-MC-2022-9** na hufanya kazi chini ya sheria ya Vyama vya Ushirika Namba **6** ya mwaka **2013** pamoja na kanuni zake za mwaka **2015**. Maeneo ya shughuli za Chama hiki ni Mkoa wa Shinyanga katika Wilaya ya Shinyanga Mjini, Shinyanga Vijijini na Kishapu.
2. Kwa idhini ya Bodi ya chama Kikuu, Mwenyekiti wa bodi anatangaza Kotesheni shindanishi ya Kitaifa (National Competitive Quotation) kwa huduma ya **UNYUNYIZAJI DAWA (FUMIGATION) MAGHALA .**

B. MAHITAJI YA KOTESHENI

KOTESHENI NA.	MAELEZO YA ZABUNI
SRCU/2026-2027/KTS/FMG/01	Zabuni ya unyunyiziaji Dawa (fumigation) Maghala kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

Chama kinatangaza : **KOTESHENI YA UNYUNYIZAJI DAWA (FUMIGATION)** katika maghala yaliyopo katika Kanda ya **KISHAPU**, Kanda ya **UZOGOLE**, na Kanda ya **SOLWA**

3. Mchakato wa Kote hii utafanyika kwa njia shindanishi ya kitaifa (National Competative Tendering) kwa mujibu wa Mwongozo wa Ununuzi na Ugavi wa vyama vya Ushirika Tanzania Bara, Sheria na Kanuni za manunuzi ya umma na ni kotesheni ya wazi kwa wazabuni wote wenye sifa zinazohitajika.
4. Kitabu cha maelezo ya kotesheni kitapatikana baada ya kulipia ada ya Zabuni kwa gharama ya Fedha za Kitanzania Shilingi Laki NNE tu (400,000) ambazo hazitarudishwa. Fedha zote zilipwe kwenye nambari ya akaunti **01J1058431301** jina la Akaunti **SHIRECU (1984) LTD Benki ya CRDB**. Ukishalipa njoo na uthibitisho wa malipo (Bank slip)
5. Waombaji wawasilishe kotesheni zao (Nakala mbili) nakala halisi moja na kopi moja zikiwa zimefungwa kwenye bahasha kwa umakini na kutiwa lakiri.
6. Muda wa kutuma maombi ya kotesheni ni siku saba 7 baada ya Tangazo kutolewa kuanzia tarehe 22 . April. 2026 hadi tarehe 28 April, 2026 saa Nne kamili asubuhi na **SIKU HIYO NDIO SIKU YA UFUNGUZI**.
7. Kotesheni zitakazochelewa hazitapokelewa wala kufanyiwa kazi wakati wa tathimini ya Zabuni bila kujali sababu zozote za kuchelewa kwazo.

C. SIFA ZA JUMLA ZA MWOMBAJI

- i. Awe Mmiliki wa Kampuni iliyosajiliwa na **BRELA** na yenye namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi [**TIN**]
- ii. Kampuni iwe na uwezo na uzoefu wa kuendesha shughuli za Fumigation
- iii. Kampuni iwe na watumishi wenye uwezo na sifa kutoka TRPI / TPHA
- iv. Kampuni iwe na vitendea kazi VIZURI vya kutosha vya kufanya kazi hiyo
- v. Kampuni iwe na Leseni hai ya kuendesha Shughuli za Fumigation
- vi. Kampuni iwe haijawahi kusababisha hasara katika kazi zake.
- vii. Waombaji wawe na kitambulisho cha NIDA.

MAOMBI YOTE YAANDIKWE KWA KUZINGATIA YAFUATAYO:

Tarehe ya mwisho kuwasilisha maombi ni siku ya **Jumanne, April 28, 2026 saa 4:00 asubuhi (Saa nne kamili asubuhi)** na **SIKU HIYO ITAKUWA NI SIKU YA UFUNGZI** utakaofanyika Makao makuu ya Ofisi ya Chama kikuu cha Ushirika [**SHIRECU (1984) LTD**], Waombaji wote mnashauriwa kuhudhuria wenyewe bila kutuma wawakilishi.

Maombi ya Kotesheni yatawasilishwa Ofisi ya Chama kikuu [**SHIRECU (1984) LTD**] yafungwe ndani ya bahasha kwa **LAKIRI** .

Barua iandikwe kwa;

**MENEJA MKUU,
SHIRECU (1984) LTD,
S. L. P. 349,
SHINYANGA.**

Kwa maelekezo zaidi kuhusiana na Zabuni hii tafadhali usisite kuwasiliana nasi kwa kupitia simu namba 0654 -174-669 au barua pepe info@shireculimited.co.tz

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA :

N.m

NAOMI MAYEGA CHABA

MAKAMU MWENYEKITI WA BODI



SHINYANGA REGION CO-OPERATIVE UNION (1984) LTD